TANGAZO LA SERIKALI Na. 236 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 217 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6, kwa-

(a) kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikisha kuwa ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (3) hadi (7) kuwa kanuni ndogo ya (2) hadi (6) mtawalia.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza, kwa-

(a) kufuta na kuandika upya Sehemu ya III kama ifuatavyo:

"SEHEMU YA III
USHURU WA KUINGIZA LORI MJINI

| **Na.** | **Chombo cha usafiri** | **Kiwango (Sh** |
|---|---|---|
| 1. | Tani 2 hadi 4 | 1,000.00 kw |
| 2. | Tani 5 hadi 9 | 2,000.00 kw |
| 3. | Tani 10 hadi 19 | 3,000.00 kw |
| 4. | Tani 20 hadi hadi 30 na zaidi | 5,000.00 kw |

(b) katika Sehemu ya X, kwa-
- (i) kufuta kipengele cha 8; na
- (ii) kubadili mpangilio wa kipengele cha 9, 10 na 11 kuwa kipengele cha 8, 9 na 10;

(c) katika Sehemu ya XX, kwa-
- (i) kufuta maneno "30% ya thamani ya eneo" katika kipengele cha 8 na badala yake kuweka maneno "10% ya thamani ya eneo"; na
- (ii) kufuta maneno "30% ya thamani ya eneo" katika kipengele cha 9 na badala yake kuweka maneno "kwa mujibu wa kiwango cha ushuru kitakachotolewa na Wizara yenye dhamana ya ardhi".

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*